NAIROBI

## Nyaribo kujitetea katika kikao cha maseneta wote

NA COLLINS OMULO GAVANA wa Nyamira, Amos Nyaribo, atajitetea mbele ya kikao cha maseneta wote dhidi ya mashtaka yaliyochangia kung'olewa afisini na Bunge la Kaunti hiyo.

Hii ni baada ya pendekezo la kuunda kamati maalum ya wanachama 11 kufeli baada ya kukosa kupata seneta wa kuliunga mkono.

Seneti imetenga kusikiliza mashtaka na utetezi wa gavana huyo kwa siku mbili kuanzia Desemba 3, 2025.

NAIROBI

## DPP afunga kesi ya mauaji dhidi ya dereva Khan

NA RICHARD MUNGUTI

Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) Renson Ingonga amefunga kesi ya mauaji inayomkabili dereva wa safari Rally, Maxine Wahome, baada ya kuwasilisha mashahidi 29.

Maxine ameshtakiwa kuhusiana na mauaji ya dereva maarufu wa mbio hizo za magari Asad Khan. Kupitia mawakili wake watatu, Maxine aliambia mahakama kwamba hana kesi ya kujibu, akisisitiza kuwa upande wa mashtaka haujathibitisha kwa ushahidi kwamba alimuua mpenzi wake wa zamani, Asad, mnamo Desemba 12, 2022.


PLUPA L-1 (r.9)

SERIKALI YA KAUNTI YA EMBU

SHERIA YA MPANGO WA MIJI NA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI
(Nambari 13 ya 2019)

NOTISI KUHUSU NIA YA KUTAYARISHA MPANGO WA MIJI NA MPANGO WA USTAWISHAJI MATUMIZI YA ARDHI

Kichwa cha Mpango wa Ustawishaji: **Mpango Shirikishi wa Ustawishaji katika Kaunti ya Embu**

Kwa mujibu wa sehemu ya 47 ya Sheria ya Mpango wa Miji na Mpango wa Ustawishaji wa Matumizi ya Ardhi ya 2019, ILANI inatolewa kwamba Serikali ya Kaunti ya Embu inanuia kuanzisha utayarishaji wa Mpango uliotajwa hapo juu mnamo Desemba 15, 2025.

Lengo la Mpango huu ni:

1. Kuweka maono kwa ukuaji na ustawishaji wa maeneo hayo ndani ya miamka 10 ijayo
2. Kutoa mwongozo jumuishi kwa ustawishaji wa Manisipaa ya Embu
3. Kuweka msingo wa ushirikishi wa utekelezaji miradi na utayarishaji bajeti na hivyo kutumika katika chombo cha usimamizi.

Shughuli katika utayarishaji wa mpango huo zitajumuisha:

1. Kuweka shughuli za matayarisho, ambayo ni jumuishi, katika manisipaa hiyo ili kutambua vipaumbele vya raia.
2. Kutayarisha mipango ya muda wa kadri na muda mrefu kuongoza muundo wa miji na ustawishaji ikiwemo mipango ya maeneo mahsusi, mipango kuhusu masuala mahsusi, mipango ya ushauri na marejeleo mengine
3. Kutayarisha mipango ya kimkakati, ikionyesha mipango ya matumizi ya ardhi iliyopendekezwa na miundo msingi
4. Kutayarisha Mpango wa Uwekezaji Mtaji (CIP)

Maoni kuhusu mpango uliopendekezwa yanaweza kuelekezwa kwa:

**WAZIRI WA KAUNTI**
**Anayesimamia Idara ya Ardhi, Madini, Nyumba, Mpango wa Miji na Ustawishaji wa Miji, S.L.P 36-60100 Embu.**
**Ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa ilani hii.**
**Tarehe: Novemba 28, 2025.**


# Rais ahimiza wanawake kujifaidi kwa mipango ya serikali

NA BENSON MATHEKA

**RAIS** William Ruto amewahimiza wanawake wa Kenya kutumia ipasavyo mipango ya serikali ya uwezeshaji inayolenga kuwaimarisha kiuchumi.

Rais alisema baadhi ya mipango ya serikali, ikiwemo Hazina ya Hustler Fund, zinafanana sana na mbinu zinazotumiwa na vikundi vya wanawake katika maeneo mbalimbali nchini.

"Nataka niwaambie wanawake ambao wana akiba katika vikundi kwamba wanaweza pia kukopa kutoka Hustler Fund kwa sababu inatoza riba ya chini na ina masharti nafuu," alisema.

Alitoa kauli hiyo alipohudhuria sherehe za kuadhimisha miaka 16 tangu kuanzishwa kwa Shirika la Joyful Women Organisation (JoyWo), ambalo mlezi wake ni Mama Taifa Rachel Ruto.

Waliohudhuria ni pamoja na Mama Rachel, Waziri wa Afya Aden Duale, Waziri wa Utalii na Sekta ya Ukarimu wa Zimbabwe Barbara Rwodzi, na Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja.

Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Kenya Commercial Bank Annastacia Kimtai na makatibu wakuu kutoka wizara mbalimbali.

Rais Ruto alifichua kuwa mtindo wa biashara wa JoyWo uliongoza kuundwa kwa Hazina ya Hustler Fund, ambayo alianzisha alipotwaa uongozi mwaka 2022.

Rais alisema alipokuwa mbunge, alijaribu mara kadhaa kuanzisha mpango wa kuwawezesha wanawake lakini akashindwa hadi Mama Rachel alipoanzisha JoyWo mwaka 2009.

"Ninasimama hapa nikiwa na fahari kusema kuwa kile kilichoanza kidogo kule Kamagut, Eldoret, leo kimekuwa harakati ya kitaifa katika kaunti 44 na wanachama 250,000," alisema.


Kwa upande wake, Mama Rachel alisema tangu kuanzishwa kwake, JoyWo imesaidia kuanzisha zaidi ya biashara 300,000 na kugusa maisha ya zaidi ya watu milioni tatu.

Aidha, alisema zaidi ya Sh4 bilioni zimekopeshwa kupitia vyama katika kaunti 44, matangi 50,000 ya kuhifadhi maji yamesambazwa kwa familia mbalimbali, na miti milioni 50 imepandwa, asilimia 70 ikiwa miti ya matunda.

"Hizi si takwimu tu. Haya ni mafanikio—hatua za mabadiliko, hatua za ujasiri, hatua za wanawake wanaokataa kubaki bila kutambuliwa," alisema.

MIPANGO | Kinara huyo wa ODM alazimika kurejea kufuatia kifo cha dada yake muda mfupi baada ya Raila Odinga kuaga

# Oburu kurejea leo nchini kupanga mazishi ya dadake


Kiongozi wa ODM Oburu Odinga akimfanyia kampeni mgombea wa ubunge Magarini, Harrison Kombe Novemba 2, 2025, kabla ya uchaguzi mdogo uliofanyika jana. PICHA|MAKTABA

**Dkt Oburu alikuwa ameenda likizoni Dubai baada ya kukosa muda wa mapumziko tangu alipompoteza ndugu yake**

NA RUSHDIE OUDIA

**KIONGOZI** wa chama cha ODM, Dkt Oburu Oginga anatarajiwa kurejea nchini leo, baada ya kukatiza mapumziko yake mafupi ili achukue tena jukumu zito la kuongoza familia ya baba yake katika kipindi kingine cha majonzi kufuatia kifo cha dada yao Beryl Achieng' Odinga, aliyefariki Jumanne.

Dkt Oburu ambaye ni msemaji wa familia hiyo aliondoka nchini Novemba 21 kuelekea Dubai kwa mapumziko, ambayo dada yake, Bi Ruth Odinga, alisema yalikuwa ya kupunguza uchovu wa kipindi kirefu cha kisiasa kilichojaa misukosuko na msongo wa hisia.

Hata hivyo, tangu kifo ch aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga mnamo Oktoba 15, 2025, familia hiyo haijapata nafasi ya kupumua. Kila siku imekuwa ni mfululizo wa wageni, viongozi, wafuasi na marafiki wanaoendelea kufurika katika mashamba ya Opoda na Kang'o ka Jaramogi kutoa pole zao.

Kifo cha Bi Achieng' kimeongeza giza katika kipindi hiki kigumu, kikizidisha uchungu wa familia na kugeuza majonzi ya awali kuwa msiba maradufu ulioshtua mno jamaa na marafiki wao.

Marafiki na jamaa wamekuwa wakifika katika mochari ya Lee kuutazama mwili huku wengine wakifika nyumbani kwake Kileleshwa kutoa rambirambi.

Akizungumza na *Taifa Leo* kwa simu, dada wa kambo wa marehemu, Bi Emily Oginga, alisema wanasubiri kurejea kwa kiongozi wa familia ili kuanza mipango ya mazishi.

"Si rahisi kwetu; ni kama msimu wa vifo umeingia kwetu. Tunasubiri Dkt Oburu ambaye anatarajiwa kuwasili Ijumaa ili tuanze mikutano ya kupanga mazishi ya dada yetu. Kwa sasa marafiki na jamaa wanaendelea kutoa pole nyumbani kwake Kileleshwa," alisema Bi Oginga.

Aliongeza kuwa wengine pia wanatembelea Kang'o ka Jaramogi kutoa pole kwa Bi Betty Oginga na Bi Susan Oginga, waliofiwa tena ndani ya muda wa miezi miwili.

Kulingana na Bw Jaoko Oburu, mwanawe Dkt Oginga, kifo cha shangazi yake kimemgusa sana kwani amepoteza mtu aliyekuwa karibu naye.

"Kwa mama yetu mpendwa na mlezi wetu Aunty B, maneno hayawezi kueleza huzuni ya kukupoteza siku 40 tu baada ya kumpoteza mlezi mwingine, Baba. Utakumbukwa sana. Tutakupenda daima na kukuenzi," alisema Jaoko.

Alisema familia ililemewa na majonzi katika wiki zilizopita, hali iliyowalazimu kumshinikiza baba yao apumzike baada ya ratiba nzito iliyomnyima muda wa kuomboleza kakake.

Familia hiyo pia imekuwa ikihudhuria shughuli nyingi za chama bila nafasi ya kiongozi huyo wa ODM mwenye umri wa miaka 82 muda wa kupumzika.

"Tumehudhuria shughuli nyingi Homa Bay, Migori na hata maadhimisho ya ODM@20. Tukagundua kuwa kiongozi wa chama hakuwa amepata hata dakika ya kuomboleza ndugu yake. Ndiyo maana tulisisitiza apate mapumziko, ambayo alichukua Alhamisi iliyopita Dubai," alisema.

Kwa bahati mbaya, msiba mwingine umepata familia kufuatia kifo cha Bi Achieng'.

# Mswada wapendekeza kampuni za kigeni ziajiri asilimia 80 ya Wakenya

NA COLLINS OMULO

**KAMPUNI** za kigeni zinazoendesha shughuli zao nchini hivi karibuni huenda zikahitajika kuhakikisha kuwa angalau thuluthi tatu ya wafanyakazi wao ni Wakenya na zinanunua malighafi na huduma kutoka nchini, ikiwa mswada ulioko bungeni utapitishwa kuwa sheria.

Mswada huo ambao umedhaminiwa na Mbunge Mwakilishi wa Laikipia Jane Kagiri, unapendekeza kuwa asilimia 80 ya wafanyakazi wa kampuni za kigeni wawe ni Wakenya.

Nafasi za usimamizi na zile za kiufundi pia zijazwe kwa msingi huo huo.

Mswada huo unaojulikana kimombo kama "Local Content Bill, 2025" unapendekeza adhabu kali, ikiwemo faini ya Sh100 milioni na kifungo kisichozidi mwaka mmoja, kwa wakurugenzi wa kampuni hizo watakaokiuka sheria hiyo.

Kulingana na mswada huo, kampuni za kigeni pia zitahitajika kununua angalau asilimia 60 ya